/ISSN 0856 – 0331X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

*No. 6* *5th June, 2026*

***SPECIAL BILL SUPPLEMENT***

*To The Special Gazette of the United Republic of Tanzania No.6 Vol. 107 Dated 5th June, 2026*
Printed by The Government Printer, Dodoma by Order of Government

# SHERIA YA KUFUTA SHERIA YA TASNIA YA PARETO YA MWAKA 2026

## MPANGILIO WA VIFUNGU

*Kifungu* *Maelezo*

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

1. Jina.
2. Fasili.

SEHEMU YA PILI
KUFUTWA KWA SHERIA YA TASNIA YA PARETO NA MASHARTI YA MPITO

3. Kufutwa kwa Sheria.
4. Uhamisho wa majukumu ya Bodi ya Pareto.
5. Uhamisho wa mali na madeni.
6. Leseni, vibali, idhini na mashauri yaliyopo.
7. Uhamisho wa watumishi.
8. Notisi ya tarehe ya kuanza kutumika.

## NOTISI

Muswada huu utakaowasilishwa Bungeni unachapishwa pamoja na maelezo ya madhumuni na sababu zake kwa ajili ya kutoa taarifa kwa umma.

Dodoma,
4 Juni, 2026

**MOSES M. KUSILUKA,**
*Katibu wa Baraza la Mawaziri*

*Muswada*
*wa*

**Sheria ya kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto na kuweka masharti kuhusu uhamisho wa mali, madeni pamoja na watumishi wa Bodi ya Pareto, kuweka masharti ya mpito na masuala mengine yanayohusiana na hayo.**

**IMETUNGWA** na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SEHEMU YA KWANZA
MASHARTI YA UTANGULIZI

Jina

**1.** Sheria hii itajulikana kama Sheria ya kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto ya mwaka 2026.

Fasili

**2.** Katika Sheria hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"mali" maana yake ni mali isiyohamishika au inayohamishika, na inajumuisha-

(a) haki zinazotokana na mkataba au makubaliano;

(b) vitabu vya hesabu na kumbukumbu; na

(c) haki, maslahi na madai mengine yoyote katika mali isiyohamishika au inayohamishika, inayoweza kuuzika au kutouzika kwa urahisi, ni dhahiri au si dhahiri, iliyoongezeka au inayoongezeka;

Sura ya 249

"Mamlaka" maana yake ni Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Usalama wa Chakula; na

"tarehe ya kuanza kutumika" maana yake ni tarehe ambayo Waziri atateua kwa mujibu wa kifungu cha 8 kwa ajili ya utekelezaji wa masuala mbalimbali yaliyoelezwa chini ya Sheria hii.

## SEHEMU YA PILI
## KUFUTWA KWA SHERIA YA TASNIA YA PARETO NA MASHARTI YA MPITO

Kufutwa kwa Sheria Sheria Na. 1 ya 1997

**3.** Sheria ya Tasnia ya Pareto ya mwaka 1997 inafutwa.

Uhamisho wa majukumu ya Bodi ya Pareto

**4.**-(1) Kufuatia kufutwa kwa Sheria ya Tasnia ya Pareto, majukumu, mamlaka na kazi ambazo kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, zilikuwa chini ya, au zinatekelezwa na Bodi ya Pareto, zinahamishwa na zitaanza kutekelezwa na Mamlaka kuanzia tarehe ya kuanza kutumika.

(2) Rejea katika sheria yoyote, mkataba, leseni, kibali, hati au nyaraka nyingine kwa Bodi ya Pareto, isipokuwa pale muktadha utahitaji vinginevyo, itachukuliwa kuwa ni rejea ya Mamlaka.

Uhamisho wa mali na madeni

**5.** Mali, wajibu na madeni yote ambayo, kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, yalikuwa yamekabidhiwa au yalitokana na Bodi ya Pareto, baada ya tarehe ya kuanza kutumika, yatakuwa chini ya, au yatasimamiwa na au dhidi ya Mamlaka.

Leseni, vibali, idhini na mashauri yaliyopo

**6**.-(1) Leseni, kibali, idhini, cheti, usajili au ridhaa yoyote iliyotolewa na Bodi ya Pareto na ambayo inaendelea kutumika kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii, itaendelea kutumika kana kwamba imetolewa na Mamlaka.

(2) Mashauri, msingi wa madai na madai yoyote, yaliyopo au yanayoendelea kabla ya kuanza kutumika kwa Sheria hii na au dhidi ya Bodi ya Pareto, yataendelezwa, kukamilishwa au kutekelezwa na au dhidi ya Mamlaka.

Uhamisho wa watumishi

**7.** Mtu ambaye, kabla ya tarehe ya kuanza kutumika, alikuwa mtumishi wa Bodi ya Pareto, baada ya tarehe ya kuanza kutumika, atakuwa mtumishi wa Mamlaka kwa vigezo na masharti yasiyopungua yale yaliyokuwa yanatumika kwake kabla ya uhamisho.

Notisi ya tarehe ya kuanza kutumika

9. Waziri, kwa notisi itakayochapishwa katika Gazeti la Serikali, atatangaza tarehe ambayo majukumu, mamlaka na kazi ambazo zinatekelezwa na Bodi ya Pareto zitahamishwa kwenda kwa Mamlaka.

---

## OBJECTS AND REASONS

---

This Bill proposes to repeal the Pyrethrum Industry Act, Act No. 1 of 1997 which was enacted with a view to provide for regulation, improvement and development of the pyrethrum industry.

The Bill is divided into Two Parts whereby; Part I deals with Preliminary Provisions which include the title of the Bill and interpretation.

Part II of the Bill provides for repeal and transitional matters whereby functions, assets, liabilities and employees of the Pyrethrum Board are transferred to and vested in the Cereals and Other Produce Regulatory Authority. The purpose of the repeal of the Pyrethrum Board is to reduce the multiplicity of regulatory bodies with related functions, to enhance coordination, improve regulatory oversight and ensure effective utilisation of public resources within the agricultural sector.

---

## MADHUMUNI NA SABABU

---

Muswada huu unapendekeza kufuta Sheria ya Tasnia ya Pareto, Sheria Na. 1 ya mwaka 1997, ambayo ilitungwa kwa lengo la kuweka masharti kuhusu udhibiti, uboreshaji na uendelezaji wa tasnia ya pareto.

Muswada huu umegawanyika katika Sehemu Mbili ambapo Sehemu ya Kwanza inahusu masharti ya Utangulizi, ikijumuisha jina la Muswada na fasili ya misamiati mbalimbali iliyotumika katika Muswada.

Sehemu ya Pili ya Muswada inaweka masharti kuhusu kufutwa kwa Sheria ya Tasnia ya Pareto pamoja na masuala ya mpito, ambapo majukumu, mali, madeni pamoja na watumishi wa Bodi ya Pareto wanahamishiwa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko. Lengo la kufuta Bodi ya Pareto ni kupunguza wingi wa taasisi za udhibiti kwa shughuli zinazofanana, kuimarisha uratibu, kuboresha usimamizi wa udhibiti na kuhakikisha matumizi yenye tija ya rasilimali za umma katika sekta ya kilimo.

Dodoma,
5 Juni, 2026

DANIEL GODFREY CHONGOLO
*Waziri wa Kilimo*